

## **Ombi kusitisha upitishwaji wa Mswada wa CyberCrime kwa hati ya Dharura**

Sisi wadau tunaowakilisha wananchi wanaotumia mtandao tunaomba Bunge lisipitishie Muswada wa Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015 kuwa sheria.

Muswada huu unaainisha makosa yanayohusiana na matumizi ya mfumo wa kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, na kuweka utaratibu wa upelelezi, ukusanyaji na matumizi ya ushahidi wa kieletroniki na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Maoni haya yanatokana na sababu zifuatazo:

1. Muswada huu haukuwekwa wazi mpaka tarehe 29 Machi na ratiba inaonyesha muswada utapitishwa chini ya hati ya dharura tarehe 31 Machi hivyo wananchi hatujapata nafasi ya kupitia kwa kina na kutoa maoni makini kuhusu muswada huo.

Ingawa muswada huu umehusisha baadhi ya wadau itambulike kuwa wadau waliitwa kwa dharura katika hatua za mwisho hivyo hawakuwa wamejiandaa kikamilifu na pia idadi kubwa ya wadau hawakuweza kuhudhuria kikao hicho kwa ajili ya kutoa maoni makini.

2. Muswada unalenga na kuhusisha kudhibiti mawasiliano ya wananchi wenyewe kwa wenyewe suala ambalo linaweza kupingana na katiba ya nchi sheria zilizopo na haki za binadamu za umoja wa mataifa.

Hivyo tunaomba kuwa kutokana na umuhimu wa muswada huu unaolenga kudhibiti uhalifu wa kimtandao, lakini kwa namna ulivyo sasa unaingilia uhuru wa mawasiliano kwa wananchi. Muswada huu usipitishwe ili kutoa nafasi kwa wananchi wengi kushiriki kikamilifu katika kuandika sheria hii muhimu.

**Ombi hili limetolewa na:**

**Irenei Kiria,**

**Kwa niaba ya Change Tanzania, Sikika na THRDC**

**Leo 29 Machi 2015**